
# Maji na Roho wanakushuhudia

**Zaburi 103, 1-3a, 3bc-4, 24ac-25, 27-28, 29-30**
**Sikukuu ya Ubatizo wa Bwana**

Eugène AMPIRE




1. Umevaa utukufu na unga**ro**,
   Umejivika mwanga kama **vazi** !
   Umetandaza anga kama **he**ma,
   Juu ya maji umejenga maka**o** yako.

2. Unafanya mawingu kuwa gari la**ko**,
   Unakwenda juu ya mabawa ya **pepo**.
   Unafanya pepo kuwa wajumbe **wa**ko,
   Na ndimi za moto kuwa watumi**shi** wako.

3. Ee Bwana, kazi zako ni nyingi sa**na**,
   Dunia imejaa viumbe **vyako**.
   Bahari iko huku, kubwa na pana **sa**na,
   Ndimo wanamokwenda bila hesabu wanyama wadogo na **wa**kubwa.

4. Wale wote wakutazamia we**we**,
   Uwape chakula wakati **wake**:
   Wewe unawapa, nao wanakio**ko**ta,
   Unafungua mkono wako, wanashi**ba** mema.

5. Ukificha uso wako, wanaangami**a**,
   Ukiondowa pumzi ya uzima, wanakufa, wanarudia mavumbi **yao**.
   Ukipeleka pumzi yako ya uzima, wanaumbwa **te**na,
   Unafanya upya uso wa **du**nia.